

USALAMA BARABARANI

Kinyanyiko: Kona kali inayogharimu maisha

Jumanne Bakana, Mwananchi
jbakana@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Kila mwezi Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani hupokea majeruhi wa ajali zinazohusisha bodaboda, bajaji na magari, huku baadhi ya matukio yakihusishwa na eneo la Kinyanyiko, ambako watumiaji wa Barabara ya Pugu-Kisarawe wanalalamikia ukosefu wa alama za barabarani.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, Dk Yonah Kabatta alisema hospitali hiyo hupokea wastani wa majeruhi watatu kwa mwezi, wanaohusishwa na ajali za bodaboda, bajaji na ajali za magari zinazotokea katika eneo hilo.

Ingawa takwimu hizo si idadi kamili ya ajali zinazotokea Kinyanyiko, ni kiashiria kuwa hospitali hiyo hupokea majeruhi wa ajali za barabarani mara kwa mara kutoka katika maeneo hayo.

"Mara nyingi huwa wanaletwa wakitokea maeneo hayo, kwa hiyo bodaboda, bajaji, mabasi na malori wanapata changamoto hapo Kinyanyiko.

"Nafikiri ile kona ni kali, kwa wale ambao hawajui njia vizuri wanajikuta wakigonga kingo za barabara," alisema.

Eneo hilo limekuwa likitajwa na watumiaji wa barabara kuwa sehemu yenye hatari kutokana na kona na mteremko mkali, huku baadhi wakisema ukosefu wa alama za barabarani unachangia ajali.

Agosti 9, 2026, watu wanne waliokuwa wakisafiri kutoka Vikumbulu kwenenda Dar es Salaam walifariki dunia baada ya basi dogo waliokuwa wamepanda kupinduka katika eneo hilo, huku wengine 46 wakijeruhiwa.

Ajali hiyo imeongeza hofu miongoni mwa watumiaji wa barabara hiyo, ambao wanasema tatizo hilo limekuwa likijirudia na linahitaji hatua za haraka kulikomesha.

Mwenyekiti wa Chama cha Bodaboda Kisarawe mkoani Pwani, Erasto Green

alisema ukosefu wa alama za barabarani ni miongoni mwa changamoto kubwa, hasa kwa madereva wanaotumia njia hiyo kwa mara ya kwanza.

"Changamoto ya hii njia yetu ya Msanga-Kisarawe, kuna ajali nyingi. Ukiangalia hakuna vile vibao elekezi katika maeneo ambayo ni hatarishi. Kwa sababu dereva ambaye amesomea anajua katika kona lazima kuwe na ishara ya kumwonyesha kilichopo mbele yake," alisema Erasto.

Dereva wa daladala anayefanya safari kati ya Kisarawe, Pwani na Gongo la Mboto mkoani Dar es Salaam, Mtalika Abeid, alisema madereva wanaoifahamu barabara hiyo wamezoea kuchukua tahadhari katika mteremko na kona za Kinyanyiko, tofauti na wageni.

"Tatizo lipo katika ule mteremko wa kutoka Minaki hadi kufika Kinyanyiko kwa sababu hakuna alama yoyote inayoonesha kona. Sisi wazoeu tunapanda na kuteremka kwa tahadhari kwa sababu tunaifahamu vizuri barabara hiyo," alisema Abeid.

Mkazi wa Kisarawe, Simon Mushi alisema ajali zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara na kuwataka mamalaka za usalama barabarani kuongeza ukaguzi wa magari na madereva.

"Madereva pamoja na vyombo vya moto vinatakiwa kukaguliwa kwa umakini. Tunapoteza ndugu zetu mara kwa mara eneo hili," alisema Mushi.

Kwa upande wake, Kaimu Msimamizi wa Idara ya Matengenezo wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Pwani, William Sungura alisema amepokea malalamiko hayo na atashirikiana na wataalamu kufanya tathmini ya eneo hilo.

"Nimepokea hiyo changamoto. Nitaongea na wenzangu kufanya tathmini kwa ajili ya kuweka hizo alama ambazo zinalamikiwa na watumiaji wa barabara hiyo," alisema Sungura.

Amewataka madereva kuchukua tahadhari wakati wote wanapotumia barabara hiyo, wakati tathmini ya mahitaji ya alama za barabarani ikiendelea.

Naye Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, William Mkonda, alisema Jeshi la Polisi linaendelea na ukaguzi pamoja na operesheni za usalama barabarani nchini kote.

"Kwa sasa bado ukaguzi unaendelea na tupo kwenye operesheni endelevu nchini kote, sambamba na utoaji elimu kwa watumiaji wote wa barabara kupitia vyombo mbalimbali vya habari na majukwaa mengine," alisema Mkonda.

Alisema Jeshi la Polisi limejikita katika kutoa elimu na kusimamia sheria kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara wanaokiuuka taratibu.

Kwa sasa, pamoja na hatua za ukaguzi na elimu, wananchi wa Kisarawe wanataka mamalaka zinazohusika kuhakikisha maeneo hatarishi kama Kinyanyiko yanawekwa alama za kutosha za kuonya madereva kuhusu kona na mteremko, ili kupunguza uwezekano wa ajali na madhara yake kwa watumiaji wa barabara.



Magari yakipanda mlima Kinyanyiko wenye kona kali kati ya Kisarawe na Pugu. Kona hiyo imesababisha ajali nyingi na watu kupoteza uhai na wengine kupata majeraha.
Picha na Jumanne Bakana

HABARILEO JUMAPILI AGOSTI 16, 2026



Pikipiki ya magurudumu matatu (toyo) ikiwa imepakia mzigo kupita urefu kinyume na sheria za usalama barabarani katika Barabara ya Kawawa, Ilala Boma mkoani Dar es Salaam jana. (Picha na Rahel Pallangyo)